

## **MAANDALIZI YA SHEREHE YA MOYO SAFI WA MAMA BIKIRA MARIA**

### **NOVENA KWA MOYO SAFI WA BIKIRA MARIA (Juni 03 - 11, 2021)**

#### **I WIMBO WA ROHO MTAKATIFU / SALA**

#### **II NIA ZA NOVENA**

- (i) Nia za Moyo Safi wa Mama Bikira Maria.
  - Kuombea Uongofu wa wakosefu
  - Kuomba Amani kwa Ulimwengu
  - Kumwombea Baba Mtakatifu na Kanisa kwa ujumla
- (ii) Kuomba kujiweka chini ya Moyo Safi wa Mama Bikira Maria.
- (iii) NIA BINAFSI

#### **III ROZARI TAKATIFU MAFUMBO YA SIKU HUSIKA**

#### **IV LITANIA YA MOYO SAFI WA MAMA BIKIRA MARIA**

#### **V MAJITOEO BINAFSI KWA MOYO SAFI WA MAMA BIKIRA MARIA**

Ee Moyo Safi wa Bikira Maria mhimidiwa! Ninakusalimu kama Moyo wa Mama wa Mungu, Mama wa Mkombozi wa wanadamu, msuluhishi wa neema zote, Malkia wa Ulimwengu na Mama yangu mpendwa.

Katika umoja na Moyo wa Yesu, Mwanao mpendwa, ninajitolea kwako kabisa bila masharti nkipaza sauti na kusema:

Ee Moyo wa Maria, mimi mzima nimali yako na yote yaliyoyangu ni yako! Ninatolea kwa Moyo wako Safi maisha yangu nashughuli zangu zote, hisi na uwezo, tunu zakiroho na kimwili, zakawaida na Kimungu, za nje na ndani, zinazopita na zinazodumu, siku zangu zilizopita, wakati wa sasa na siku zijazo bila masharti, muda wangu, uhai, uzima wa milele, moyowangu, mwili, roho, nafsi na asili yangu kabisa – yote!

Ee Moyo Safi wa Mama yangu, utawale juu yangu na unitumie mimi na sadaka yangu kadiri ya mipango namapenzi yaMungu.

Ee Moyo wenye kuwaka Upendo wa Mungu, ninakutegemea wewe kabisa na kujiaminisha kwako. Uwe nuru nanguvu yangu, tegemeo langu na msaada wangu, pumziko na kimbilio langu, furaha yangu na uzima wangu, msuluhishi nayote yangu baada ya Moyo Mtakatifu wa Yesu, Mfalme na Mpenzi wangu.

Ninakuahidi, ee Moyo Safi, kwa mfano wako kuepuka dhambi zote na dosari ambazo kama miiba mikali zingeweza kukuumiza.

Ninatamani ili tangu sasa kila saa ya maisha yangu iwe tendo safi la upendo kwa Yesu lenye kutendeka katika umoja na Moyo wako safi, ee Maria.

Ninataka kuishi na kufanya kazi, kusali na kuteseka, kupambana na kufa kwaajili ya kuharakisha ujio wa utawala wa Moyo wa Yesu kupitia kwa utawala wa Moyo wako wa kimama.

Ee Moyo wa Bikira Mwaminifu na kimbilio la wakosefu, nifanye niwe mwanafunzi na mfuasi mwaminifu wa Yesu. Uamshe ndani mwangu chuki ya dhambi na fikra za dunia hii. Unijalie roho ya utoto wa Kimungu wenye kuunganishwa na Utatu Mtakatifu, ili kwa maombezi yako tayari hapa duniani nifikie kiwango kile cha utakatifu na katika uzima wa milele kiwango kile cha utukufu ambacho Mungu alinitayarishia tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Amina

VII    Moyo Mtakatifu wa Yesu ..... Utuhurumie X 3

Moyo Safi wa Mama Bikira Maria ..... Utuombee X3

VIII    TUNAKIMBILIA ULINZI WAKO

## **NYIMBO:**

### **ITWAUSIFU MOYO WAKO MARIA**

**Twausifu, moyowako Mama Maria, (moyomwema )  
Twauheshimu, moyowako mama Maria (moyosafi)  
Moyowako Maria usionadoa, Moyowako Maria usionadoa.**

- 1 Moyowako MAMA unafaraja/ Unang'arasanaunavyopendeza  
Moyowako MAMA mpenzi Maria/ Ni msafikweliunameremeta
- 2 Moyowako MAMA, umekingiwa/ Dhambiyaasilituliyoirithi  
Moyowako MAMA nimiratifu/ Umejaaneemanemateletele
- 3 Moyowako MAMA, kamawaridi/ Unafurahishaunametameta  
Moyowako MAMA, kamadhahabu/ Ing'arayosanamfanowakioo
- 4 Moyowako MAMA, nimtiisana/ Moyowako MAMA mtulivukabisa  
Moyowako MAMA ninurunjema/ ItuongozayokufikaMbinguni
- 5 Moyowako MAMA, nimnyenyeketu/ Moyowako MAMA unaheritele  
Moyowako MAMA niwa Amani/ Moyowako mama unaneemayaMungu
- 6 Tuombee MAMA yetu Maria/ Tuombee MAMA kwamwanaoYesu Ili  
atakasemioyoyetu/ Ifananenawe MAMA yetumpenzi

## **2.MOYO WA MARIA TUOMBEE**

**(K) Moyosafi (moyosafi) wa Maria; Moyomwema (moyomwema)  
wa Maria, moyowa Maria tuombee X 2**

- 1 Moyowako Maria, moyo wahuruma, moyo unaotupenda sisi wanawako, utuombee msamaha kwaYesu (mo-oyo)
- 2 Moyowako Maria, wauvumilivu, uliopata uchungu pale msalabani utuombee sisi wakosefu (mo-oyo)
- 3 Moyo wako Maria, moyo waneema utujalie faraja sisi wenye dhambi, tupate tumaini kuokoka (mo-oyo)
- 4 Moyowako Maria, Mama wamwokozi, ututie nguvu katika maisha yetu tumtumikie vema muumba wetu (mo-oyo)

Avee Maria! Mapendo ni ya Milele. “....imewapasa kumwomba Mungu siku zote....”(Lk. 18:1)